

**WAZIRI MAHIGA AFANYA ZIARA KATIKA VITIVO VYA SHERIA VILIVYOPO  
MKOANI MOROGORO 17 MACHI, 2020**



*Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Augustine Mahiga, akifafanua jambo wakati wa kikao cha kujadili tasnia ya sheria nchini kilichofanyika mkoani Morogoro , tarehe 17 Machi, 2020*



*Kaimu Mkuu wa "Law School of Tanzania" Dkt. Zakayo Lukumay akifafanua jambo kwa baadhi ya wakufunzi wakati wa kikao hicho 17 Machi, 2020*

## ***Na Scholastica Njozi – Law School of Tanzania***

---

Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Augustine Mahiga akiongozana na Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome na Naibu Katibu Mkuu Bw. Amon Mpanju (wote wa Wizara ya Katiba na Sheria) na Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (The Law School of Tanzania) Dkt. Zakayo Lukumay na Dkt. Nyika ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Elimu ya Sheria Nchini (Council for Legal Education), wamefanya ziara katika vitivo vya Sheria katika vyuo vya Mzumbe, Chuo cha Kiislamu Morogoro na Chuo cha Jordan vya mkoani Morogoro.

Akiwa katika vitivo hivyo, Waziri Mahiga alifanya vikao vya pamoja ili kujadili mustakabali wa Tasnia ya Sheria nchini kwa lengo la kuona ni kwa namna gani inachangia katika kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa kati kupitia mapinduzi ya viwanda ili kuunga juhudi za Mhe. Rais Joseph Magufuli. “ Mtambue kuwa hawa wanafunzi wanaotoka hapa wanakwenda kutoa na kusimamia haki kwa raia hivyo ni lazima kuwa makini na mnachokifundisha.” Anasema Mahiga. Aidha ametaka wakufunzi kuangalia namna ya kuboresha mafunzo kwa sababu kumekuwa na tofauti kati ya wanasheria wa zamani na wa sasa.

Akizungumza katika vikao hivyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Prof. Sifuni Mchome amesema vyuo viangalie namna vanavyotoa mafunzo ili kuendana na Tanzania ya uchumi wa kati na mapinduzi ya viwanda na Tasnia ya Sheria haiwezi kuachwa nyuma katika hili. Prof. Mchome anasema “ Katika harakati za kuipeleka nchi katika uchumi wa kati hakuna mtu anayepaswa kuachwa nyuma na kama kuna changamoto zozote basi ni jukumu letu sote kulitafutia ufumbuzi”.

Naye mjumbe wa Baraza la Elimu ya Sheria (CLE) amesema wao wana jukumu kubwa la kusimamia elimu ya sheria nchini na kwa sasa wapo katika mchakato wa kufanyia kazi changamoto zilizoainishwa na wadau mbali mbali ili kuona kama mtaala uliopo una mapungufu yapi ili yaweze kurekebishwa.

Naye Dkt. Zakayo Lukumay amesema kuwa, wanafunzi wote wanaomaliza shahada zao za sheria katika vyuo hivyo wote hupita “Law School”. Na kumekuwa na malalamiko juu ya ufaulu wao lakini baada ya Taasisi kufanya utafiti wamebaini matatizo ya wanafunzi hayo yanapaswa kutatuliwa kwa ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo wakuu wa vitivo vya sheria, Wizara ya Elimu. Akiwasilisha andiko lake

katika vikao hiyo, Lukumay amesema kuna uhusiano mkubwa kati ya ufaulu katika ngazi ya elimu sekondari, ufaulu wa shahada na hata ufaulu wa law school. Aidha, aliweka wazi kuwa, mwanafunzi aliyefaulu vizuri masomo yake ya sekondari na chuo kikuu, huwa na nafasi nzuri ya kufaulu pia katika mitahini ya Law School.

Katika kikao hicho, wote kwa pamoja wamekubaliana kila Kitivo cha Sheria kuandika andiko linaloonyesha changamoto zilizo katika Tasnia hii ya Sheria na namna ya kuzitatua. Andiko hilo linatakiwa kuwasilishwa kwenye Wizara ya Katiba na Sheria kwa hatua mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuitisha kikao cha pamoja cha wadau kwa ajili ya majadiliano na mapendekezo zaidi.



**Waziri wa Katiba na Sheria Dkt Augustine Mahiga (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wakufunzi wa Chuo Kikuu Cha Jordan cha Mkoani Mororogo alipofanya ziara tarehe 17 Machi, 2020.**